**Katekisimu ya Kanisa la Kimethodisti Ulimwenguni**

Sehemu ya 1: Kauli ya Lengo

Maana ya Kauli ya Katekisimu: Katekisimu ni mpangilio wa kielimu *na* kikanuni wa mafundisho ya kanisa. Ni zana ya kiimani na kielimu ya kuwaelekeza watu katika maisha kamili ya kanisa *na* dhihirisho rasmi la mafundisho muhimu ambayo kanisa hutarajia washirika wake kuelewa na kuamini. Kwa hivyo, kujifunza katekisimu kunapaswa kutazamwa, pamoja na ubatizo na kukiri imani, kama hatua muhimu ya kuwaidhinisha Wakristo katika ushirika wa kanisani.

Lengo la Mchakato wa Katekisimu: Lengo la katekisimu ni kuwapa mafunzo washirika wapya ili wafahamu, wakumbuke, wakiri na wafurahie mafundisho muhimu ya kanisa. Hii ni pamoja na kiini cha kanuni za msingi za kidini za Kanisa la ulimwengu pamoja na ahadi za msingi za mafundisho ya dhehebu.

Hafla za Katekisimu: Mchakato wa katekisimu unapaswa kutumika kwa washirika wote wapya kanisani. Hatua hii inaweza kutokea kama sehemu muhimu katika safari kutoka ubatizo wa watoto hadi kipaimara, kama sehemu inayohitajika katika ugeuzaji na ubatizo wa watu wazima, au kama hatua inayohitajika kwa washirika wapya (waliobatizwa awali) wanaojiunga kwenye dhehebu. Katika hali ambapo waumini wote wanajiunga kwenye dhehebu, wakleri wanatarajiwa kuongoza kila kanisa la mtaa kupitia mchakato wa katekisimu.

Sehemu ya 2: Kanuni za Mpangilio

Katekisimu imepangwa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu kanuni za kiekumene, msingi wake ukiwa Imani ya Nikea. Sehemu ya pili inahusu Sifa za Imani Ya Wesley.

Sehemu ya 3: Vyanzo vya Kauli za Katekisimu

Kwa sababu katekisimu ni mpangilio wa kikanuni wa mafundisho ya kanisa, vyanzo vyake vikuu vinapaswa kuwa viwango vya kiimani vya kanisa. Katika *Kitabu cha Mafundisho na Nidhamu ya Kanisa la Kimethodisti Ulimwenguni*, tunakiri ari ya "kuendelea kuwa imara na thabiti katika maandiko na katika mafundisho ya kihistoria ya Kanisa la Kikristo kama ilivyoelezwa katika Vipengele vya Dini na Kanuni ya Imani, na kueleweka kupitia mtazamo wa imani wa Wesley" (¶ 103). Katekisimu hii imepangwa na kutolewa kwenye vyanzo hivyo.

1. Maandiko Matakatifu — "Vitabu rasmi vya Agano la Kale na Jipya (kama ilivyobainishwa katika Vipengele vya Dini) ndivyo sheria na mamlaka ya msingi ya imani, maadili, na huduma, ambako mamlaka mengine yote hupimwa" (¶ 104). Kama ilivyotajwa katika *Kanuni ya Imani*, kuwa "Tunaamini Biblia Takatifu, Agano la Kale na Agano Jipya, ufunuo wa Neno la Mungu kadiri inavyohitajika kwa wokovu wetu. Inapaswa kupokelewa kwa njia ya Roho Mtakatifu kama sheria na mwongozo wa kweli wa imani na matendo. Chochote ambacho hakijafunuliwa au kuthibitishwa na Maandiko Matakatifu hakipaswi kuwa kifungu cha imani wala kufundishwa kuwa muhimu kwa wokovu" (Kifungu cha IV). Katika sehemu zote, katekisimu hii inatoa marejeleo kwa maandiko yanayofunua na kuthibitisha mafundisho tunayokiri hapa.
2. Imani ya Nikea — Pamoja na Imani ya Mitume (takriban mwaka wa 250 BK) na Tafsiri ya Maana ya Kalsedoni (451 BK), Imani ya Nikea (381 BK) ni ya kanisa la ulimwengu. Hivi ni viwango vya kiimani vya kudumu na visivyoweza kubadilishwa (¶ 105). Imani ya Nikea ndiyo muundo wa msingi na chanzo cha Kanuni za Kiekumeni za katekisimu hii.
3. Vipengele vya Dini na *Kanuni ya Imani* (CoF) — "[Z]ote mbili, Vipengele vya Dini na Kanuni ya Imani, vinabainisha mipaka ya mafundisho ya kanisa letu" na "kuonyesha msisitizo na masuala ya kipekee ya kanisa letu, pamoja na urithi wa kidini wa imani yetu" (¶ 106). Viwango hivi vinathibitisha mwafaka wa kiekumeni na pia vinafafanua Njia ya wokovu ya Wesley. Viwango hivyo ni muundo wa msingi na chanzo cha Sifa za Imani ya Wesley katika katekisimu hii.

4. Njia ya Wokovu ya Wesley — Njia ya Wokovu ya Wesley iliyobainishwa katika Vipengele vya Dini na Kununi ya Imani ndiyo msingi wa urithi wa kidini wa imani ya Wesley na imefafanuliwa mwanzoni mwa *Kitabu cha Mafundisho na Nidhamu* ¶ 102. Ufafanuzi wa neema ya Mungu katika Sifa za Wesley za katekisimu hii hufuata Njia ya wokovu ya Wesley.

Sehemu ya 4: Katekisimu

A. *Kanuni za Kiekumeni*

**Tunamwamini Mungu mmoja, Baba, Mwenyezi, muumba wa mbingu na nchi, na vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.**

*1. Je, unamwamini Mungu?*

Ndiyo. Ninamwamini Mungu, Baba, Mwenyezi, muumba wa mbingu na nchi, na vyote vinavyoonekana na visivyoonekana. (Mwa. 1:1-31; 17:1; Yosh. 2:11; Zab. 8:3-8; Isa. 42:5; 1 Wakor. 8:6; Waef. 4:6; Waebr. 1:5; Ufu. 4:11; CoF I.)

*2. Mungu ni nani?*

Mungu ndiye Mungu wa kweli, mtakatifu na aliye hai, Roho wa Milele, Utatu Mtakatifu. (Kumb. 6:4; Wal. 19:2; Yer. 10:10; Math. 28:19; Yoh. 17:3; Waebr. 9:14.)

*3. Ni nini maana ya fumbo la Utatu Mtakatifu?*

Mungu ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, tofauti lakini wasioweza kutenganishwa, daima pamoja katika asili na uwezo. (Luka 3:21-22; Yohana 15:26; Matendo 2:33; War. 8:9-11; 2 Wakor. 13:13; Wagal. 4:4-6; Waef. 2:18; Tito 3:4-6; Waebr. 9:14; 1 Pet. 1:2; CoF I.)

*4. Mungu ni Mwenyezi kwa njia gani?*

Mungu ana uwezo, hekima, haki, wema, na upendo bila mwisho. (Ayubu 12:13; 42:2; Zab. 89:14; 107:1; Isa. 55:9; Yer. 32:17; Math. 19:26; Luka 1:37, 18:7; Warumi 5:8, 11:33-36, 16:27; 1 Yohana 4:7-16; CoF I.)

*5. Uhusiano wa Mungu na mbingu na nchi ni upi?*

Mungu ni Muumba, Mtawala na Mlinzi wa vitu vyote. (Mwa. 1:1-31; Kumb. 4:39; 1 Waf. 8:23; Neh. 9:6; Zab. 8:1; Meth. 16:9; Isa. 44:24; Matendo. 17:24; War. 8:28; Ufu. 4:11; CoF I.)

*6. Mungu hutawala vipi mbingu na nchi?*

Mungu hutawala kwa neema akizingatia ustawi na wokovu wa wote, kwa utukufu wa jina lake. (Kutoka 34:6; Zab. 104:31, 116:5; Yoe. 2:13; Mik. 7:18-20; Yoh. 3:16; Waef. 2:4-7; 2 Pet. 3:9; CoF I.)

**Tunamwamini Bwana mmoja, Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa kwa Baba tangu milele, Mungu kutoka kwa Mungu, Mwanga kwa Mwanga, Mungu kweli kwa Mungu kweli, aliyezaliwa bila kuumbwa, mwenye Uungu mmoja na Baba; kupitia Kwake vitu vyote viliumbwa.**

*7. Je, unamwamini Yesu Kristo?*

Ndiyo. Ninamwamini Bwana mmoja, Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu. (Marko 9:7; Math.

3:17; Yohana 3:16; Matendo 2:36; War. 10:9; 1 Wakor. 8:6; Wafil 2:11; Yuda 1:4)

*8. Je, Mwana ni Mungu?*

Ndiyo. Mwana amezaliwa kutoka kwa Baba tangu milele, Mungu kutoka kwa Mungu, Mwanga kwa Mwanga, Mungu kweli kwa Mungu kweli, aliyezaliwa bila kuumbwa, mwenye Uungu mmoja na Baba. (Luka 10:22; Yohana 1:1, 14, 18; 8:12; 10:30; Wafilipo 2:6; Wakol. 1:15, 19; 2:9; Waebr. 1:1-5.)

*9. Jukumu la Mwana katika uumbaji ni lipi?*

Kupitia kwake vitu vyote viliumbwa. (Yohana 1:3; 1 Wakor. 8:6; Wakol. 1:16-17; Waebr. 1:2.)

**Kwa ajili yetu na wokovu wetu Alishuka toka mbinguni, akafanyika mwili kupitia Roho Mtakatifu na Bikira Maria na akawa mwanadamu kweli.**

*10. Kwa nini Mwana wa Mungu akawa mwanadamu?*

Kwa ajili yetu na wokovu wetu. (Yohana 3:17; 14:6; Matendo 4:12; 16:30-31; War. 3:21-26; 10:9; Tito 3:6-7; Waebr. 7:25.)

*11. Mwana wa Mungu alikuwa mwanadamu vipi?*

Alishuka kutoka mbinguni, akafanyika mwili kupitia Roho Mtakatifu na Bikira Maria na akawa mwanadamu kweli. (Math. 1:18; Luka 1:30-35; Yohana 1:1-2, 14; War. 1:3-4; Wagal. 4:4; Wafil 2:6-8; 1 Yohana 1:1-3, 4:2.)

*12. Yesu Kristo ni nani?*

Mwana wa Mungu na Bwana wetu Yesu Kristo ni nafsi moja ambape ndani asili ya uungu na ubinadamu zimeunganishwa kikamilifu na haziwezi kutenganishwa. (Isa. 9:6; Math. 1:20-23; Yohana 1:14, 14:9-11; War. 1:3-4; Wakol. 1:15-20; 1 Tim. 3:16; Waebr. 1:1-3; CoF II.)

**Kwa ajili yetu Alisulubiwa kwa mamlaka ya Pontio Pilato; Akateswa, Akafa na Akazikwa. Siku ya tatu Alifufuka kutoka wafu, kama ilivyo katika Maandiko; Akapaa mbinguni na ameketi kuume kwa Baba. Atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu wazima na wafu, na ufalme Wake hautakuwa na mwisho.**

*13. Mungu anatupatanisha vipi ndani ya Kristo?*

Mungu hutupatanisha kwake kupitia kifo cha Kristo msalabani. (Math. 27:26, 50, 59-60; Marko 15:15, 37, 45-46; Luka 23:23-25, 46, 53; Yohana 19:16, 30, 33-34, 38-42; War. 3:21-26; 5:6-11; 1 Wakor. 15:3-4.)

*14. Je, Yesu Kristo alifufuka kimwili kutoka kwa wafu?*

Ndiyo! Siku ya tatu Alifufuka kutoka kwa wafu, kama ilivyo katika Maandiko. (Math. 28:1-10; Marko 16:1-8; Luka 24:1-11, 36-43; Yohana 20:1-17, 27; Matendo 2:22-36; 1 Wakor. 15:3-8, 1 Pet. 1:3.)

*15. Je, Yesu Kristo ni Bwana wa mbingu na nchi?*

Ndiyo. Alipaa mbinguni na ameketi kuume kwa Baba. Atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu wazima na wafu, na ufalme Wake hautakuwa na mwisho. (Luka 1:33, 24:51; Yohana 5:22-29; Matendo 1:9-11;

10:42; War. 8:34; 2 Wakor. 5:10; Wafil. 2:9-11; 2 Pet. 1:11; Ufu. 11:15.)

16. *Je, Yesu Kristo ni kuhani mkuu?*

Ndiyo. Kwa kuwa Yesu anaishi milele, ana hadhi ya kuhani wa milele. Kwa hiyo, anaweza kuwaokoa kabisa wale wanaomjia Mungu kupitia kwake, kwa sababu daima anaishi kuwaombea. (War. 8:34; Waebr. 4:14-16; 7:11-28; 1 Yohana 2:1-2.)

17. *Ni nani atahukumiwa?*

Watu wote watahukumiwa kwa haki na Yesu Kristo sasa na siku ya kiama. (Math. 7:21-23; 25:31-46; Yohana 5:22-29; Matendo 10:42; 17:30-31; 2 Wakor. 5:10; CoF XII.)

18. *Je, tunafanywa wenye haki kupitia matendo yetu?*

Hapana. Hatuwezi kufanywa wenye haki kindani wala kuhesabiwa kama wenye haki mbele za Mungu kupitia matendo au sifa zetu. (Luka 5:32; War. 3:21-30; 4:2-5; 11:6; Wagal. 2:15-16; Waef. 2:8-10; Tito 2:14; 3:4-7; 1 Yohana 1:9; CoF IX.)

19. *Tunawezaje kuepuka ghadhabu ya Mungu?*

Mungu huthibitisha, au kuwabainisha wenye dhambi wanaotubu na wanaokiri imani kwa Bwana wetu Yesu Kristo kuwa watu wenye haki. (Yohana 3:36; War. 3:21-30; 4:6-8; 5:6-11; Waef. 1:7-14; 2:3-7; 5:5-10; Wakol. 3:5-17; 1 Wathes. 5:8-10; CoF IX.)

**Tunamwamini Roho Mtakatifu, Bwana, mleta uzima, atokaye kwa Baba na Mwana, ambaye pamoja na Baba na Mwana anaabudiwa na kutukuzwa, aliyenena kupitia manabii.**

20. *Je, unamwamini Roho Mtakatifu?*

Ndiyo. Ninamwamini Roho Mtakatifu, Bwana, mleta uzima. (Isa. 11:2; 61:1; 2 Wakor. 3:17-18.; Yohana 6:63; War. 8:11; Wagal. 6:8.)

21. *Je, Roho Mtakatifu ni Mungu?*

Ndiyo. Roho hutoka kwa Baba na Mwana, na pamoja na Baba na Mwana anaabudiwa na kutukuzwa. (Math. 28:19-20; War. 8:9; 1 Wakor. 2:9-11; 3:16; Wagal. 4:6)

Amenena kupitia manabii. (2 Sam. 23:2; Isa. 61:1-3; Zek. 7:12; Math. 1:22-23; Waebr. 1:1-2; 1 Pet. 1:10-12; 2 Pet. 1:20-21.)

22. *Roho Mtakatifu hutuelekeza vipi kwa toba?*

Hushawishi ulimwengu wa dhambi, haki na hukumu. (Mik. 3:8; Yohana 16:7-11; CoF III.)

23. *Je, wokovu unaweza kupatikana bila Roho Mtakatifu?*

Hapana. Roho Mtakatifu hutuelekeza kuchukua hatua ya kiimani katika injili na kutuleta kwenye ushirika wa Kanisa. (CoF III) (Yohana 3:3-6; War. 8:9-17; Waef. 2:17-22; Tito 3:4-7.)

24. *Roho Mtakatifu hufanya kazi vipi Kanisani?*

Huwafariji, kuwatunza na kuwawezesha waaminifu na kuwaongoza katika ukweli wote. (Yohana 14:25-26; 16:12- 15; War. 8:2-6, 12-17, 26-27; 1 Wakor. 12:4-11; Wagal. 5:16-25; CoF III.)

25. *Ukweli kuhusu wokovu unapaswa kupatikana wapi?*

Tunaamini Biblia Takatifu, Agano la Kale na Agano Jipya, ufunuo wa Neno la Mungu kadiri inavyohitajika kwa wokovu wetu. (Zab. 119:105, 130; Math. 4:1-4; 2 Wathes. 2:15; 2 Tim. 3:16-17; CoF IV.)

26. *Tunapaswa kupokea Maandiko vipi?*

Biblia Takatifu inapaswa kupokelewa kupitia Roho Mtakatifu kama sheria na mwongozo wa kweli katika imani na matendo. (Methali 30:5-6; Yak. 1:21-25; 1 Pet. 1:23-25; 2 Tim. 3:16-17; CoF IV.)

**Tunaamini katika kanisa moja takatifu katoliki na la mitume.**

27. *Je, unaamini katika kanisa?*

Ndiyo. Ninaamini katika kanisa moja, takatifu, katoliki, na la mitume. (Yohana 10:16; 1 Wakor. 12:12-13; Waef. 4:4-6; 5:25-27; 1 Pet. 2:9-10; Ufu. 5:9-10.)

28. *Kanisa hujumuisha akina nani?*

Kanisa la Kikristo ni jamii ya waumini wote wa kweli chini ya Utawala wa Kristo. (Math. 28:19-20; 1 Wakor. 1:2-3; Waef. 2:11-22; Ufu. 7:9-10; CoF V.)

29. *Kanisa ni nini?*

Ni ushirika wa ukombozi ambapo Neno la Mungu linahubiriwa na walio na wito wa kiungo, na sakramenti zinatolewa ipasavyo kulingana na uteuzi wa Kristo mwenyewe. (Yer. 1:5; Matendo 2:41-47; 1 Wakor. 11:23-27; CoF V.)

30. *Kwa nini kanisa lipo?*

Kwa nidhamu ya Roho Mtakatifu, kanisa lipo kwa ajili ya kudumisha ibada, kuboresha tabia za waumini na ukombozi wa ulimwengu. (1 Wakor. 12:27-28; 14:12; Wagal. 6:1-2, 6-10; Waef. 4:11-16; Waebr. 3:12-14; 10:23-25; CoF V.)

31. *Je, ni sawa na vyema kumwabudu muumba na mkombozi wetu?*

Ni jukumu na haki yetu kuinama ili kusujudu, kwa unyenyekevu na kwa heshima katika uwepo wa Mungu. (Zab. 92:1-2; 95:1-7; 103:1-5; 107:1; Wafil. 2:9-11; Ufu. 4:11; 5:9-14; CoF XIII.)

32. *Kwa nini imani ni muhimu kwa maisha ya kanisa?*

Mikusanyiko ya watu wa Mungu kwa ajili ya ibada ni muhimu kwa ajili ya Ushirika wa wakristo na ukuaji wa kiroho. (Matendo 2:41-47, 4:31; Warum. 1:11-12; Waebr. 10:23-25; CoF XIII.)

**Tunatambua ubatizo mmoja kwa ajili ya ondoleo la dhambi.**

33. *Je, unaamini kwamba kuna ubatizo mmoja tu?*

Ndiyo. Ninatambua ubatizo mmoja kwa ajili ya ondoleo la dhambi. (Waef. 4:4-6.)

*34. Ubatizo ni nini?*

Ubatizo unaashiria kuingia katika familia ya imani na ni ishara ya toba na utakaso wa kindani dhidi ya dhambi, dhihirisho la kuzaliwa upya katika Yesu Kristo na alama ya ufuasi wa Kikristo. (Matendo 2:37-39; War. 6:1-5; 1 Wakor. 12:12-13; Wagal. 3:27-28; Wakol. 2:11-14; Waebr. 10:19-22; CoF VI.)

**Tunatazamia ufufuo wa wafu, na uzima wa ulimwengu ujao. Amina.**

*35. Tumaini letu kuu ni lipi?*

Tunatazamia ufufuo wa wafu, na uzima wa ulimwengu ujao. (Yohana 6:39-40; 11:25-26; War. 6:5-8; 8:22-23; 1 Wakor. 15:20-23, 50-55; Wafil. 3:10-12, 20-21; 1 Wathes. 4:13-18.)

*36. Matokeo mawili ya hakika yanayowakabili wanadamu ni yepi?*

Wenye haki watafufuka wapate uzima wa milele na waovu watapata hukumu ya milele. (Math. 13:24-30, 36-43; 25:31-46; Yohana 5:25-29; Ufun. 20:11-15; 21:1-8; 22:1-5; CoF XII.)

B. *Sifa za Imani Ya Wesley*

*37. Je, sababu, utamaduni, au uzoefu ni mwongozo wa kutosha kwa mafundisho ya Kikristo?*

Hapana. Chochote ambacho hakijafunuliwa au kuthibitishwa na Maandiko Matakatifu hakipaswi kufanywa kuwa kifungu cha imani wala hakipaswi kufundishwa kuwa muhimu kwa wokovu. (Isaya 40:8; 2 Wafal. 17:15; War. 1:21; Waef. 4:17-18; Wakol. 2:8; 2 Tim. 3:16; CoF IV.)

*38. Sakramenti ni nini?*

Sakramenti ni ishara na ahadi za imani ya Mkristo na upendo wa Mungu kwetu. (Marko 14:22-24; Math. 26:26-28; Luka 22:19-20; Yohana 6:53-59; Matendo 2:38; Wagal. 3:27; 1 Wakor. 10:15-17, 11:23-25; CoF VI.)

*39. Je, Sakramenti ni ishara pekee?*

Hapana. Ni mbinu za neema ambazo Mungu hutumia kufanya kazi bila kuonekana ndani yetu, kuharakisha, kuimarisha na kuthibitisha imani yetu kwake. (Yohana 6:53-58; War. 6:3-4; 1 Wakor. 10:15-17; Wakol. 2:12; 1 Pet. 3:20-21; CoF VI.)

*40. Kuna Sakramenti ngapi?*

Sakramenti mbili zimetawazwa na Kristo Bwana wetu, yaani ubatizo na Meza ya Bwana. (2 Waf. 5:14; Isa. 44:3; Ezek. 36:25-27; Marko 14:22-24; Math. 26:26-28; 28:19; Luka 22:19-20; Yohana 3:5; 6:53-58; Matendo 22:16; CoF VI.)

*41. Tunaweza kuwabatiza watoto?*

Ndiyo. Tunaamini kwamba watoto wako chini ya msamaha wa Kristo na kama warithi wa Ufalme wa Mungu ni watu wanaokubalika kwa Ubatizo wa Kikristo. (Luka 18:15-17; Matendo 10:44-48; 16:15, 30-

34; 18:8; 1 Wakor. 1:16; CoF VI.)

*42. Je, Ubatizo unatosha kuleta wokovu?*

Hapana. Watoto waliobatizwa wanapaswa kulelewa na kuongozwa hadi wamkubali Kristo kivyao, na kwa kukiri imani wathibitishe Ubatizo wao. (Kumb. 6:20-25; Marko 16:16; Yohana 1:12; 3:16; Matendo 2:38; 16:29-34; War. 10:9-11; CoF VI.)

*43. Nini maana ya Meza ya Bwana?*

Meza ya Bwana ni mbinu ya neema, dhihirisho la ukombozi wetu, ukumbusho wa mateso na kifo cha Kristo, na ishara ya upendo na muungano ambao Wakristo wanao kwa Kristo na kati yao. (Marko 14:22-24; Math. 26:26-28; Luka 22:19-20; Yohana 6:53-59; 1 Wakor. 10:16-17; 11:23-25; Wagal. 3:27; CoF VI.)

*44. Tunakutana vipi na Kristo katika Meza ya Bwana?*

Wale wanaoshiriki mkate uliomegwa na kunywa kikombe kilichobarikiwa ipasavyo, kwa njia inayostahili na kwa imani wanashiriki mwili na damu ya Kristo kwa njia ya kiroho mpaka atakaporudi. (Luka 24:28-32; Yohana 6:53-58; 1 Wakor. 11:23-29; CoF VI.)

*45. Je, kuna mbinu nyingine za neema?*

Ndiyo. Miongoni mwa mbinu hizo ni maombi na kusoma Maandiko. (Math. 7:7-8; Luka 11:13, 18:1-5; Yohana 5:39; Matendo 17:11-12; 2 Tim. 3:15-17; Yakobo 1:5, 5:13-18.)

*46. Asili ya ubinadamu ni ipi?*

Tunaamini kwamba mwanadamu ameanguka kupoteza haki na, mbali na neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, hana utakatifu na anafanya maovu. (Mwa. 6:5; Zab. 51:5; Mhub. 9:3; Yer. 17:9-10; War. 3:23; 5:12-14; Waef. 2:1-3; 1 Yohana 1:8; CoF VII.)

*47. Tunawezaje kujiokoa kwenye hofu ya hali hii?*

Hapana. Kwa uwezo wetu wenyewe, bila neema ya kiungu, hatuwezi kufanya matendo mema yanayompendeza na kukubaliwa na Mungu. (Zab. 51:5; Yohana 6:63; War. 7:14-24; Wagal. 5:17; Waef. 2:1; CoF VII.)

*48. Basi ni nani anayeweza kuokolewa?*

Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu mambo yote yanawezekana. (Math. 19:26; Yohana 3:5, 16, 36; 5:24; 6:40; 8:51; 11:25-26; War. 5:8; Wagal. 2:21; Waef. 2:1-10; 2 Tim. 1:9; Tito 3:5.)

*49. Mungu hutuokoa vipi?*

Kupitia neema yake inayozuia, kushawishi kuhakikisha, kutakasa, na kutukuza. (War. 2:14-16; 3:21-26; 5:15; 6:14; 2 Wakor. 5:17; Wagal. 2:21; Waef. 2:8-9; Wafil. 2:12-13; 2 Tim. 1:9; Tito 2:11-14; 3:4-7; Waebr. 10:22; 1 Pet. 4:10; 5:10; 1 Yoh. 3:9)

*50. Neema hufika vipi katika nafsi zilizotamauka?*

Neema ya Mungu ya inayoongoza (mwongozo) hupunguza athari za dhambi ya asili hata kabla

hatujagundua umuhimu wa Mungu. (Kumb. 4:37; 7:6-8; 14:2; Math. 5:45; Luka 15:20; Yohana 6:44; 15:5; 2 Pet 3:9; Tito 2:11-12; D&D §102.)

*51. Neema inayoongoza hupunguza vipi athari za dhambi ya asili?*

Inazuia athari zote za kutengwa kwetu na Mungu na kuhuisha dhamiri, ikitupa hisia ya awali ya Mungu na mwelekeo wa kwanza kwa maisha kamili. (Luka 24:45; Yohana 6:37; 12:32; Matendo 16:14; War. 8:7-8; 1 Wakor. 2:14; D&D §102.)

*52. Neema inayoongoza hurejesha vipi uhuru wa maamuzi?*

Tukiwa katika hali ya kufungwa na kutamauka, neema inayoongoza huingilia na kutuwezesha kuchukua hatua za kweli za neema ya ziada ya Mungu. (2 Wafalme 6:17, 20; Yohana 16:8-11; Matendo 2:37; 8:31; 15:8; 16:30; D&D §102.)

*53. Je, Mungu hubainisha matendo yote ya binadamu?*

Hapana. Wanadamu wakiwa wamewezeshwa na kushawishiwa na Roho Mtakatifu, wana uhuru wa kutumia maamuzi yao kwa wema. (Mwa. 2:16-17; Kumb. 30:15-20; Yosh. 24:14-15; 2 Nya. 7:14; Isa. 55:6-7; Math. 16:24; Marko 1:17; Yohana 1:12-13; 7:17; War. 10:8-9; 1 Wakor. 10:13; 2 Pe 3:9; Ufun. 3:20; CoF VII.)

*54. Wokovu ni Nini?*

Tukisema wokovu tunamaaanisha, zaidi ya ahadi ya uzima wa milele, lakini pia ukombozi wa sasa kutoka kwa dhambi, urejesho wa nafsi kwa utakaso wake halisi; kurejeshwa hali ya kiungu; katika wema na utakatifu wa kweli, kwa haki, rehema na ukweli. [1] (War. 5:10; 2 Wakor. 5:17; Wagal. 5:22-25; Tito 2:11-12, 3:5; 1 Petro 2:24; 1 Yohana 1:9, 2:2.)

*55. Mungu hutuelekeza kwa toba vipi?*

Neema ya Mungu ya kushawishi huamsha ndani yetu hamu ya kuepuka ghadhabu ijayo na kutuwezesha kuanza kumcha Mungu na kutenda haki. (Hos. 6:1; Mik. 4:1-2; Habak. 2:4; Zek. 8:20-23; Yohana 16:8; Waef. 2:4-5; 2 Wakor. 7:9-10; Waebr. 13:18; D&D §102.)

*56. Mungu hutupatanishi vipi kwake mwenyewe?*

Neema ya Mungu ya yenye haki hufanya kazi kwa imani ili kuleta upatanisho na Mungu kupitia kafara ya msamaha wa Yesu Kristo. (Isa. 53:4-6, 12; Yohana 3:16; War. 5:10-11; 2 Wakor. 5:18-19; Waef. 2:13-16; Wakol. 1:19-20; Waebr. 2:17; D&D §102.)

*57. Je, kafara ya msamaha wa Kristo hufikia wanadamu wote?*

Ndiyo. Sadaka aliyoitoa Kristo msalabani kwa hiari ni kafara kamilifu na ya kutosha kusafisha dhambi za ulimwengu mzima. (Mwa. 12:3; Isa. 56:8; Yohana 1:29; 3:16-17; 5:24; 8:12; 11:25; 12:32; War. 8:11; 2 Wakor. 5:14-15; 1 Tim. 2:3-6; Waebr. 2:9; 10:12; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 1:9; 2:2; CoF VIII.)

*58. Je, Mungu anahitaji kafara nyingine yoyote?*

Hapana. Sadaka ya Kristo inatukomboa dhidi ya dhambi zote, hivyo hakuna kafara nyingine inayohitajika. (Kumb. 10:12- 13; War. 3:21-26; 1 Tim. 2:5-6; Waebr. 10:12-14; CoF VIII.)

*59. Haki hii hufanya nini?*

Kunatupa msamaha wa dhambi. (Mwa. 15:6; Zab. 32:1-2; Yohana 1:29; War. 1:16-17; 4:6-8; 5:9; Waebr. 9:26; 1 Pet. 1:18-19; 2:24; 1 Yohana 2:2; 4:10; D&D §102.)

*60. Tunawezaje kuhakikishiwa msamaha huu?*

Roho wa Mungu hushuhudia pamoja na roho zetu kwamba sisi ni watoto wa Mungu. (War. 8:15-17; Wagal. 3:26; 4:6-7; Waef. 1:13-14; 2 Tim. 1:7; Waebr. 10:15-17; D&D §102.)

*61. Je, wokovu ni msamaha na hakikisho tu?*

Hapana. Kwa kuzaliwa upya, Mungu hutufanya upya katika haki kupitia Yesu Kristo, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. (Ezek. 36:26-27; 1 Wakor. 2:14-16; Wagal. 2:20; 5:16-25; Waef. 2:1-5; Tito 3:4-7; 2 Pet. 1:4; CoF IX.)

*62. Tunabadilishwa vipi katika kuzaliwa upya?*

Tunashiriki asili ya kiungu na kufurahia maisha mapya. (Mwa. 15:6; 17:5; 35:10; Yohana 3:3; War. 8:1; 2 Wakor. 5:17; Wagal. 5:22-24; Wakol. 3:2-3; 2 Pet. 1:3-4; 1 Yohana 4:4; CoF IX.)

*63. Kuzaliwa upya hutuwezesha vipi kuishi kama watoto wa Mungu?*

Kwa kuzaliwa upya, mwumini anapatanishwa na Mungu na kuwezeshwa kumtumikia yeye kwa hiari na mapenzi yake. (Mwa. 15:6; Kumb. 6:5; 10:12-13; Yohana 1:12; War. 8:16-17; 2 Wakor. 6:18; Wagal. 3:26; 4:4-7; Waef. 1:5-6; Wafili. 2:13; 1 Yohana 3:1, 10; CoF IX.)

*64. Je, tunaweza kupoteza wokovu wetu?*

Ndiyo. Tunaamini kuwa, ingawa tumezaliwa upya, inawezekana kuacha neema na kuingia katika dhambi. (Yohana 15:1-6; 1 Wakor. 9:27; 10:11-12; 2 Wakor. 11:3; War. 11:19-22; Wagal. 5:4; 1 Wathes. 3:8; 1 Tim. 1:18-20; 4:1-2; 5:15; 2 Tim. 3:1-5; 4:3-4; Waebr. 2:1-4; 3:12-14; 6:1-6; 2 Pet. 2:1-3, 20-21; 3:17; Ufun. 2:4-5; 3:11; CoF IX.)

*65. Je, waliopoteza neema watahukumiwa milele?*

Hapana. Hata hivyo, kwa neema ya Mungu, wanaweza kufanywa wapya katika haki. (Kum. 4:29-31; 30:1-4; Zab. 51:12; Amosi 9:14; War. 8:35-39; Wagal. 6:1; Yak. 5:19-20; Yuda 22-23; Imani IX.)

*66. Tunaweza kuwa na imani pasipo matendo?*

Hapana. Tunaamini kwamba matendo mema ni matunda muhimu ya imani na yanafuata kuzaliwa upya lakini hayaondoi dhambi zetu wala hayatuepushi kwenye hukumu ya Mungu. (Math. 7:21; Yohana 14:15; War. 2:13; Waef. 2:8-10; Yak. 1:22-25; 2:14-18, 26; CoF X.)

*67. Neema ya Mungu huendelea kufanya kazi vipi ndani yetu kupitia Neno na Roho Mtakatifu?*

Neema inayotakasa ya Mungu husafisha dhambi tunazofanya kupitia mawazo, maneno na matendo yetu, na kutuwezesha kuishi kulingana na mapenzi ya Mungu. (Zab. 51:2, 7-12; Yer. 31:31-34; Eze. 36:25-27; Wagal. 5:16-25; Tito 2:11-14; 1 Yoh. 1:7, 9; CoF XI.)

*68. Utakaso huendelezwa vipi katika maisha ya kila siku?*

Utakatifu wa moyo na maisha (Wal. 20:26; Amosi 5:14; War. 6:22, 12:1; 2 Wakor. 7:1; Waebr. 12:14; 1 Pet. 2:5, 9), unaojumuisha matendo ya uchaji wa Mungu (War. 12:12, 15:4; 1 Wakor. 11:23-26; 1 Wathes. 5:16-18; Waebr. 10:24-25; Yak. 5:13-16) na matendo ya huruma (Kumb. 15:10-11; Zab. 82:3-4; Meth. 19:17; Isa. 61:1; Mika 6:8; Math. 19:21, 25:31-46; Luka 11:42; Mdo. 2:44-45; War. 12:13).

*69. Neema inayotakasa hutufanyia nini kingine?*

Hutuwezesha kujitahidi kupata utakatifu huo ambao lazima tuwe nao ili kumwona Bwana. (Math. 6:33; Yoh. 17:17; War. 8:29; 12:1; 2 Wakor. 3:18; 7:1; Waef. 4:22-24; Wakol. 1:21-22; 1 Wathes. 5:23; 2 Wathes. 2:13; Waebr. 6:1- 3; 12:14; 1 Pet. 1:13-16; 1 Yohana 3:2-3; 5:3; CoF XI.)

*70. Je, utakatifu wa kweli unawezekana?*

Ndiyo. Utakaso kamili ni hali ya upendo kamili, haki, na utakatifu wa kweli ambao kila mwumini aliyezaliwa upya anaweza kuupata. (Kut. 19:6; Wal. 11:44-45; 19:2; Kumb. 7:6; 14:2; Math. 5:43-48; 1 Yohana 3:2-3; 5:3; CoF XI.)

*71. Umuhimu wa utakaso kamili ni upi?*

Ni kukombolewa dhidi ya uwezo wa dhambi; kumpenda Mungu moyo, nafsi, akili, na nguvu zote; na kumpenda jirani yako kama unavyojipenda. (Walaw. 19:18; Kumb. 6:5; Marko 12:30-31; War. 13:9-10; Wagal. 5:13-14; 1 Wathes. 5:23; CoF XI.)

*72. Je, utakaso kamili huja hatua kwa hatua au mara moja?*

Kupitia imani katika Yesu Kristo zawadi hii ya neema inaweza kupokelewa katika maisha haya hatua kwa hatua au mara moja. (Meth. 4:18; Matendo. 15:9; Waefe. 4:15; 1 Wathes. 5:23-24; 1 Pet. 2:2; 2 Pet. 3:18; CoF XI.)

*73. Je, kila mtu anapaswa kutafuta utakaso kamili?*

Ndiyo. Unapaswa kutafutwa kwa bidii na kila mtoto wa Mungu. (Wal. 19:2; Zab. 86:11; Waebr. 12:14; 1 Pet. 1:13-16; 2 Pet. 1:3-11; CoF XI.)

*74. Je, utakatifu hutukomboa dhidi ya udhaifu wa maumbile ya kibinadamu?*

Hapana. Tunaamini kuwa utakaso huu hautukomboi dhidi ya udhaifu, ujinga, na makosa ya kawaida ya mwanadamu, wala hauondoi uwezekano wa kutenda dhambi zaidi. (Zab. 86; 1 Wakor. 10:12; 2 Wakor. 12:7-9; Wagal. 6:9; Waebr. 3:12-15; 10:26-39; Ufu. 2:2-7; CoF XI.)

*75. Tutatunza baraka hii vipi?*

Ni lazima tuitikie mapenzi ya Mungu kikamilifu ili dhambi ipoteze uwezo wake dhidi yetu; na ulimwengu, mwili, na ibilisi awekwe chini ya miguu yetu. (Kum. 30:19-20; Yosh. 24:15; Zab. 37; Meth. 3:5-8; Math. 8:18-22; Marko 8:34-38; War. 12:1; 16:20; Yak. 4:8; CoF XI.)

*76. Tunawezaje kupata ushindi dhidi ya ulimwengu, mwili, na ibilisi?*

Kwa uangalifu kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu. (Kumb. 6:16-19; Math. 24:36-51; 25:1-13; Luka 21:34-36; 1 Pet. 1:13-16; 5:8-9; CoF XI.)

*77. Kazi ya mwisho ya neema ndani yetu ni ipi?*

Tumaini na ahadi yetu kuu katika Kristo ni utukufu, ambapo nafsi na miili yetu itarejeshwa kikamilifu. (Isa. 26:19; Dan. 12:2-4; Yohana 11:25-26; War. 6:5; 8:22-23; 1 Wakor. 15:35-56; Wafil. 3:20-21; Ufu. 21:1-5; D&D §102.)